# RASIMU YA KATIBA YA
# TANZANIA SHARING ASSOCIATION

**Dira ya chama chetu:**

1. Kusaidiana katika shida na raha (Social Issues).
2. Kufanya mambo ya maendeleo na ustawi wa wanachama (Development Issues).
3. Kusaidia kutatua matatizo madogo madogo yatakayohitaji msaada katika jamii.

# APRIL 2025

# IBARA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Tanzania Sharing Association ni chama cha watanzania wenye **ASILI au NASABA** ya utanzania kwa kuzaliwa, kuoa au kuolewa, na jambo lingine lolote linaloweza kumpa haki ya uraia (kisheria) mtu anayejitambulisha kama mtanzania kwa kukili na kujitambua kuwa ni mtanzania, kuadaptiwa au kuzaliwa na mtanzania. Chama hiki kilianzishwa jijini Houston katika Jimbo la Texas tarehe **4/1/2019**. Baada ya mwaka mmoja, wanachama walikubaliana kukubali ndugu, jamaa na marafiki waishio majimbo tofauti ndani ya USA.

# IBARA YA PILI

## 2. JINA NA CHAMA

Jina la chama hiki litafahamika kama **Tanzania Sharing Association,** na kifupisho chake kitajulikana kama **TSA**.

# IBARA YA TATU

## 3. USAJILI, ANUANI, NA NEMBO YA CHAMA

### 3.1 Usajili:

Chama hiki kimesajiliwa kama shirika lisilo na faida (Non profit Organization), vilevile kitakuwa ni chama huru kisicho cha serikali na kisichofungamana na chama chochote cha siasa, jamii, kabila na wala misingi ya dini yoyote. Chama kitaendesha shughuli zake kwa mujibu wa katiba na sheria za Texas.

### 3.2 Anuani:

Ofisi ya chama itakuwa Houston Texas na itatumia anuani ya posta

PO BOX 720801
Houston, TX 77072
No. ya simu: (206) 602-0506

Anuani hii itatumika mpaka hapo chama kitapofungua ofisi.

3.3 **Nembo ya Chama**

## IBARA YA NNE

**4. NIA NA MADHUMUNI YA CHAMA**

4.1 Kujenga moyo wa upendo na ushirikiano kwa taratibu, kanuni na sheria zilizowekwa baina na wanachama.

4.2 Kutiana moyo katika masuala yote yahusuyo elimu, biashara, kazi, taaluma na ustawi wa jamii kwa ujumla.

4.3 Kwa kuzingatia ibara ya 4.1, wanachama watapaswa kuzingatia yafuatayo:

Kusaidiana wakati wa shida. Hii itajumuisha masuala yote ambayo yanaweza kumfika mwanachama au ndugu waliokuwa kwenye mkataba kama **msiba.**

- Ugonjwa – Kwa mwanachama, mume/mke na watoto iwapo watakuwa mahututi (Life threatening condition) na kukaa hospitali mfululizo kwa muda wa zaidi ya majuma mawili.
- Kushikiliwa na uhamiaji na kuunguliwa na moto – ni kwa mwanachama tu.
- Katibu/Mhakiki ataomba nakala kama cheti cha kuzaliwa, nakala kutoka kwa daktari, nakala kutoka shule, nakala kutoka police, nakala kutoka kituo cha zima moto, nakala kutoka chumba cha kuhifadhia maiti n.k ili kuridhia nakutangaza shida hizo.
- Mwanachama atatakiwa kutoa taarifa za shida/msiba ndani ya siku 7.
- Mwanachama atasaidiwa kuandaa sherehe/maombi kwa kiasi cha **($300)** kama kutakuwa na sherehe/maombi kwa ajili ya shida/msiba.
    - Mwanachama anatakiwa kutoa taarifa siku 7 kabla ya sherehe hiyo na ndani ya siku 40 toka shida/msiba kutangazwa.
    - Mwanachama hatakabidhiwa pesa bali kiongozi husika atashirkiana na mwanachama kusimamia shughuli hiyo.

4.4 Kwa kuzingatia ibara ya 4.3, ndugu wanaokubalika ni kama wafuatayo:

- Wazazi/walezi wawili – Wazazi wa mwanachama au walezi wa mwanachama kama shangazi/mjomba/bibi/babu/binamu/wakwe.
- Mume/mke mmoja – Mume/mke unaeishi naye, baba/mama watoto, rafiki unaeishi naye (boyfriend/girlfriend).
- Watoto – Wakuzaa mwenyewe, wa mume/mke, wa kaka/dada/mtoto aliefariki.
- Kaka/dada – Wa tumbo moja au wa baba (wakufikia).

4.5 Kwa kuzingatia ibara ya 4.3 jumla ya shida/msiba ni **5** ndani ya miaka **5** ukiwemo msiba mkubwa wa mwanachama na mtoto wa chini ya miaka 21 aishio USA.

- Shida/msiba ya ndugu alieandikishwa na wanachama zaidi ya mmoja, kipaumbele kitatolewa kwa mwanachama mwenye shida/misiba michache au kwa makubaliano yatakayofanyika na wanachama hao**.**

**Wanachama Wapya**

- Idadi ya shida/msiba ndani ya mwaka itategemeana muda wa mwanachama kuwa hai na ikitokea kama kuna shida/msiba kabla muda wake basi itatangazwa KIHIARI. Mwaka utaanza rasmi pale mwanachama atapofikisha miezi 6.

**Wanachama wa Zamani**

- Idadi ya shida/msiba ndani ya mwaka itategemeana muda wa mwanachama kuwa hai na ikitokea kama kuna shida/msiba kabla muda wake basi itatangazwa KIHIARI.
- Ikitokea msiba/shida zaidi ya 1 ndani ya miezi 3, mwanachama atatangaziwa na kuchangiwa shida/msiba mingine baada ya miezi 3 (baada ya msiba kutokea).

**Uangalizi:** Hakutakuwa na ubadilishaji wa ndugu au kuongezwa isipokuwa watoto/dada/kaka watakaozaliwa. Watoto wa kaka/dada au mtoto aliefariki. Mume/mke na watoto wao wanaweza badilishwa iwapo mume/mke hawajachangiwa. Na ikitokea wana watoto sio wakuwazaa, watoto wa mume/mke anayebadilishwa watatakiwa kuondolewa kwenye mkataba.

# IBARA YA TANO

**5. UANACHAMA**

5.1 **Chama hiki kitajumuisha wanachama wafuatao**

- Wanachama waanzilishi.
- Wanachama waanzilishi waliohama USA.
- Wanachama wapya watakaojadiliwa na kukubaliwa na wanachama kwa asilimia isiyopungua 75 ndani ya siku 3.
- Wanachama wenye kupatwa na maradhi ya muda mrefu na kushindwa kushiriki kwa kutoa michango (Miezi 6).

5.2 **Sifa za Uanachama**

- Awe na akili timamu.
- Awe na umri usiopungua miaka 21.
- Akubaliane na kanuni na masharti mbali mbali kama yalivyoainishwa na katiba, sheria na nyaraka nyingine za chama.
- Awe na mahusiano mazuri pamoja na viongozi/wanachama wenzake.

5.3 **Namna ya kujiunga na Chama**

- Mwanachama atatakiwa kutoa kiingilio cha **$100**, akiba tangulizi ya kiasi cha **$100**, na kiasi cha **$25** kila mwaka.
    - Kiingilio cha $100 na kiasi cha $25 kila mwaka hazirejeshwi kwa mwanavhama (Non refundable).
- Chama kitaendelea kupokea wanachama wapya mara moja kwa mwezi (Tarehe 1 ya mwezi).
- Uanachama utaanza rasmi pale mwanachama atakapotia saini kwenye nakala zote na kukubalika na kiongozi husika.
    - Nakala hizo zitakaguliwa na kukubalika ndani ya siku 10 tangu siku ya kutangazwa.

5.4 **Ukomo wa Uanachama:**

- Mwanachama kufariki.
- Kujihudhuru mwenyewe kwa hiari.
    - Mwanachama atatakiwa kumuandikia Mwenyekiti ujumbe na sababu ya kujitoa.
    - Atashauriwa na mwenyekiti nakupewa masaa 72 ya kuamua.
    - Atapatiwa barua ya kujitoa/kutolewa katika chama.
    - Atatakiwa kurudisha pesa yote aliochangiwa kutoa pesa aliochanga (**yote au $50 kila mwezi**).

- Hatorudishiwa pesa ikiwa mchango wake ni mkubwa kuliko alivyochangiwa.
- Hatoruhusiwa kurudi kwenye chama mpaka muda wa **mwaka mmoja** na kuanza kama mwanachama mpya.
  - Iwapo mwanachama ana deni, atatakiwa kurudisha deni hilo kabla ya kukubalika.

- Kufukuzwa uanachama iwapo ataonekana kupoteza sifa za uanachama.
  - Atatakiwa kurudisha pesa yote aliochangiwa kutoa pesa aliochanga (**yote au $50 kila mwezi**).
  - Atarudishiwa akiba yake tangulizi (advance).
  - Hatoruhusiwa kurudi kwenye chama mpaka muda wa **mwaka mmoja** na kuanza kama mwanachama mpya.
    - Iwapo mwanachama ana deni, atatakiwa kurudisha deni hilo kabla ya kukubalika.

## 5.5 Sababu za kusimamishwa uanachama na adhabu zake

### 5.5.1 Mwanachama atasimamishwa iwapo atafanya yafuatayo:

- Kutoheshimu uongozi na wanachama wote.
- Kutuma matangazo siku sizizo za matangazo zaidi ya mara 3.
- Kuleta mambo binafsi kwenye chama.
- Kutumia lugha isiyo sahihi na kuanzisha malumbano yasihusiana na chama.
- Kushabikia mambo binafsi na kuendeleza malumbano zaidi ya mara 3.
- Kutawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na chama nnje ya chama.
- Mwanachama akihukumiwa na vyombo vya sheria kwa makosa yanayotishia amani ya wanachama (kama unyanyasaji wa kijinsia, unyanyasaji wa nyumbani, biashara ya ngono, ulevi, kushughulika na madawa ya kulevya, kuua kwa kusudia).
- Kujitoa (Exit) kwenye chama wakati wa mkutano.
  - Atakuwa na mkutano na Bodi ya Wadhamini na kupewa maamuzi.

### 5.5.2 Mwanachama atapewa warning zifuatazo:

- Kutaarifiwa kama amekosea na Afisa Uhusiano.
- Kuandikiwa barua na Mwenyekiti.
- Kuwa na mkutano na Bodi ya Utendaji.
  - Kutolewa kwenye chama kwa muda wa siku 30.
  - Kupewa taarifa zote kuhusiana na michango na kuchanga kama kawaida.
  - Kuruhusiwa kutoa taarifa za Shida/Msiba na kuchangiwa kama kawaida.

**Uangalizi:** Mwanachama huyu akirudia makosa na kusimamishwa zaidi ya mara 2, atatolewa kwenye chama na kutoruhusiwa kurudi kwenye chama.

## IBARA YA SITA

### 6 HAKI NA WAJIBU WA WANACHAMA

6.1 **Kila mwanachama anayo haki ya:**

- Kuwepo katika orodha ya wanachama.
- Kuangalia rekodi zote za chama kama vile taarifa za vikao vilivyopita, mikataba n.k.
- Kuhoji kuhusu mapato na matumizi ya chama.
- Kugombea nafasi za uongozi.
- Kunufaika na chama kwa mujibu wa katiba, kanuni na sheria.
- Haki sawa ya kuchangia mawazo ya uendeshaji wa chama kwa mujibu wa katiba, kanuni na sheria.
- Kutoa malalamiko ili yajadiliwe kwa uwazi na kupewa ufumbuzi ndani ya chama.
- Kupiga kura iwapo kura zitahitajika.

6.2 **Kila mwanachama anatakiwa awajibike kama ifutavyo:**

- Kuzifahamu, kutii na kuzifuata kanuni na sheria za chama.
- Kutumia lugha sahihi na kutoanzisha malumbano yasiohusiana na chama.
- Kulinda na kutunza heshima na amani ya chama kwa viongozi na wanachama.
- Kutunza na kutotawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na chama.
- Kutoa michango na ada kulingana na mahitaji na mienendo ya chama.
- Kujitoa kwa hali na mali, pamoja na muda wake katika kuhakikisha malengo ya chama yanaafikiwa.
- Kuhudhuria na kushiriki kikamilifu vikao vyote vitakavyo itishwa na chama (Vikao vinaweza kuwa vya online/whatsap, simu au kukutana).
- Kuchangia ufahamu na uzoefu kwa faida ya chama, wanachama wake na jamii inayozunguka chama hiki.
- Kutoa taarifa kwa viongozi anapohama au kusafiri kwa muda mrefu, anapobadili anuani, number ya simu, barua pepe na warithi.
- Kutoa taarifa za shida/msiba kwa kiongozi husika ili kuendelea na mchakato.

- Kuhakikisha ana kiasi cha $125 kwenye account ndani ya siku 30 ili kupatiwa pesa/rambirambi anayotakiwa kupatiwa katika kipindi cha siku 7 ya kutoa taarifa ya shida.
    - Akiba tangulizi (advance) kwa ajili ya kukaa kwenye akauti ya chama ($100).
    - Pesa ya uanachama kila mwaka ($25).
        - Kila mwanachama atatakiwa kutoa $25 kila mwezi wanne (April).
        - Mwanachama atakaekuwa hana akiba tangulizi (advance) ya kutosha (less than $100) wakati wa shida/msiba na kupelekea TSA kuazima pesa kwa TSA Investment klabu, atatakiwa kulipia **10%** ya pesa itakayoazimwa na kutangazwa wakati wa msiba.

# IBARA YA SABA

## 7 MUUNDO WA CHAMA

Muundo wa uendeshaji wa chama utakuwa wa ngazi tatu za vikao/mikutano kama ufuatavyo:

### 7.1 Mkutano Mkuu

Kutakuwa na mkutano mkuu wa chama utakaofanyika mara moja kwa mwaka (March). Maamuzi yataafikiwa kwa wingi wa kura za wanachama.

#### 7.1.1 Majukumu ya mkutano mkuu:

- Kuchagua viongozi wa chama ikiwa muda wa uchaguzi umefika.
- Kupokea taarifa ya utendaji wa chama na mipango ya mwaka unaofuata.
- Kupokea taarifa za mapato na matumizi kwa mwaka mzima.
- Kufanya marekebisho kwenye miongozo na vifungu mbali mbali vya katiba ikiwa muda wa marekebisho umefika.
    - Katiba itarekebishwa tena baada ya miaka 2.

### 7.2 Mkutano wa Kamati ya Utendaji

Kutakuwa na mikutano itakaofanyika mara moja kwa kila baada ya miezi mitatu. Maamuzi yataafikiwa kwa wingi wa kura za viongozi wa kamati ambao ni lazima kura zisiwe chini ya asilimia 50 (50%).

### 7.2.1 Majukumu ya mkutano wa kamati ya utendaji:

- Chombo kikuu cha kusimamia masuala yote ya kila siku ya chama.
- Kuandaa, kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mipango ya chama.
- Kuandaa na kufanya maboresho ya kanuni na taratibu mbalimbali zitakazotumika kuendesha chama na kuwasilisha kwa Bodi na wanachama.
- Kusimamia taratibu na kanuni za chama.
- Kuwasilisha taarifa za utendaji, utekelezaji na maendeleo ya chama kwenye mkutano mkuu wa chama.
- Kujadili maombi ya wanachama wapya.
- Kupokea, kujadili na kutoa mapendekezo ya mabadiliko ya katiba kama itakavyo jitokeza.
- Kujadili na kupendekeza agenda kwa ajili ya mkutano wa nwisho wa mwaka.

## 7.3 Mkutano wa Bodi

Kutakuwa na mikutano itakaofanyika mara tatu kwa mwaka. Maamuzi yataafikiwa kwa wingi wa kura za wajumbe wa Bodi ambao ni lazima kura zisiwe chini ya asilimia 50 (50%).

### 7.3.1 Majukumu ya mkutano wa Bodi:

- Kushauriana na kutatua matatizo yatakayojitokeza kwenye chama.
- Kupokea taarifa ya utendaji wa chama na mipango inayofuata.
- Kushughulikia masuala yanoyohusu wanachama/viongozi yanayojitokeza.
- Kujadili mapendekezo na hoja tofauti zinazohusiana na chama.
- Kubadilisha au kurekebisha vipengele vya katiba pale inapohitajika kwa kushauriana na wanachama.
- Kujadili na kupendekeza agenda kwa ajili ya mkutano wa mwisho wa mwaka.
- Kusitisha uanachama/uongozi kama utajitokeza.

**Uangalizi:** Mikutano ya dharura inaweza kufanyika kwa ngazi zote tatu pale ambapo itaonelea umuhimu wa kufanyika. Agenda, mahali/aina ya mkutano na muda vitatolewa mapema na Mwenyekiti/Makamu wa Mwenyekiti.

## IBARA YA NANE

**8 UTARATIBU WA KUENDESHA MIKUTANO**

- Mikutano yote itatolewa taarifa ya kufanyika ndani ya siku kumi na nne (14) kabla ya kufanyika.
- Agenda pendekezwa zitawekwa wazi kwa wanachama wote ili wenye agenda za ziada waweze kuziwakilisha kwa Mwenyekiti kwa uchambuzi na mapitio siku tatu (3) kabla ya kikao.
- Vikao vya dharura kwa kamati zote vinaweza kuitishwa kulingana na mahitaji pasipo kigezo cha kutoa taarifa rasmi katika kipindi kilichowekwa.
- Muhutasari wa kikao utaandaliwa na kusomwa kwenye mkutano au kikao kikuu.

## IBARA YA TISA

**9 TARATIBU ZA KUPIGA KURA KATIKA UCHAGUZI**

- Kura zitapigwa kwa siri/wazi iwapo kutakuwa na mpinzani.
- Kila mwanachama hai atakuwa na haki ya kupiga kura moja kwa mgombea mmoja.
- Endapo ikatokea kura kulingana mara mbili mfululizo, Mwenyekiti ana haki ya kutumia kura ya turufu ili mshindi aweze kupatikana.
- Mgombea/Mada yeyote lazima apate/ipate kura nyingi zaidi ya wengine/nyingine ili kuweza kutangazwa kwa ushindi.

## IBARA YA KUMI

**10. UONGOZI WA CHAMA**

10.1 **MKURUGENZI MTENDAJI**

10.2 **KAMATI YA UTENDAJI**

- MWENYEKITI
- KATIBU/MHAKIKI
- MWEKA HAZINA
- AFISA UHUSIANO

10.3 **BODI YA WADHAMINI**

- MWENYEKITI
- KATIBU
- WAJUMBE (3)

## 10.4 VIONGOZI WA KLABU

Kwa kuzingatia ibara ya 10, Klabu hizi zitafanya kazi na kuongozwa na viongozi kama ifuatavyo:

- **BURUDANI (Entertainment)**
  Klabu hii hushughulika na maandalizi ya sherehe za chama. Sherehe hizi ni kwa ajili ya wanachama wote pamoja na sherehe za klub. Klabu hii itaongozwa na viongozi si zaidi ya watatu na itakuwa ikisaidia Klabu zingine au wanachama watakaohitaji msaada kwenye shughuli zao.

- **RAHA (Enjoyment)**
  Klabu hii ni ya wanachama watakaopenda kujiunga na kufata sheria watakazojiwekea. Klabu hii ni kwa ajili ya kufurahi kwa pamoja hasa kwenye birthdays, baby shower, harusi, bridal showers na kadharika.

- **WATOTO (Kids)**
  Klabu hii ni ya watoto wa umri kati ya mwaka mmoja (1) mpaka miaka kumi na mbili (12) ambao watakuwa wakikutana mara moja kwa mwaka hasa kipindi cha kiangazi (Summer). Klabu hii ina malengo yafuatayo:
    - Kufahamiana.
    - Kucheza kwa pamoja.
    - Kujifunza mila na desturi za Kitanzania/Kimarekani.

- **VIJANA (Teens)**
  Klabu hii ni ya vijana wenye umri kati ya miaka 13 mpaka 20 ambao hukutana mara kwa mara kwenye mtandao wa ZOOM kwa lengo la kujifunza mambo mbalimbali ya kijamii. Vijana hawa watakuwa wakikutana mara moja kwa mwaka hasa kipindi cha kiangazi (Summer) kwa malengo ya:
    - Kufahamiana.
    - Kucheza kwa pamoja.
    - Kujifunza mila na desturi za Kitanzania/Kimarekani.

- **UDHAMINI (Sponsorship)**
  Klabu hii ni ya vijana wanaomaliza shule ya sekondari (high school) na Itaongozwa na kamati maalumu. Vijana watakaohitimu watatakiwa:
    - Kushiriki katika klabu ya vijana
    - Kuonyesha sifa za kuwa kiongozi
    - Kuwa na GPA ya 3.0.
    - Kuandika Insha (Essay) ya mada itakayotolewa na kamati.
    - Kukubalika na chuo chochote kinachotambulika.
    - Kuwa mtoto wa mwanachama/wanachama hai.

- **VIJANA WAKUBWA (Young Adult)**
  Klabu hii ni ya Vijana wenye umri kati ya miaka 21 mpaka 30 watakaopenda kujiunga na kufata sheria watakazojiwekea. Klabu hii ina malengo yafuatayo:
    - Kufahamiana.
    - Kubadilishana mawazo.
    - Kushirikiana katika shughuli na mipango mbali mbali ya maendeleo.

- **UWEKEZAJI (Investment)**
  Klabu hii ni ya mwanachama yeyote wa TSA atakaependa kujiunga na kuwekeza kwenye miradi mbali mbali. Wanachama hawa watakubaliana na kufata sheria watakazojiwekea. Makusanyo na mapato yanajadiliwa na wanachama wa Klabu na si vinginevyo. Klabu hii kwasasa inawekeza kwenye ukopeshaji kwa riba ndogo na inategemea kuja kuwekeza kwenye mambo mbali mbali yanayousiana na jamii kwa ujumla.

**Uangalizi:** klabu zote zitakuwa chini ya uangalizi wa viongozi wake na Mwenyekiti. Viongozi wa Klabu zote watawakilisha shughuli husika na zitategemea michango ya wanachama, ndugu, jamaa na marafiki. Iwapo kutahitajika msaada, chama kitajaribu lusaidia kitakapoweza.

## IBARA YA KUMI NA MOJA

### 11. SIFA NA MUDA WA UONGOZI

#### 11.1 Sifa za Kiongozi

- Anatakiwa kuwa mwanachama hai kwa muda usiopungua **miezi 6** na kwa mwanachama mwenye **ASILI au NASABA** ya utanzania kwa muda usiopungua **miezi 12**.
- Atakayeweza kusoma, kuzungumza na kuelewa kiswahili na kingereza.
- Anatakiwa kukubalika na viongozii/wanachama kwa wingi wa kura.
- Kutambua kuwa vikao vinaendeshwa kiswahili.
- Kuhakikisha ana pesa kwenye akaunti ya chama kama akiba.
- Kuwa mwaminifu, mvumilivu, jasiri, kujiamini, na kuwa na maono ya vitu mbalimbali.
- Kuwajibika kwa kutenda kazi na kujitolea.
- Kuongoza kwa kuonyesha mifano ya utendaji.
- Kukubaliana na wengi wape na kushirikiana sio vinginevyo.
- Kutokuwa na ubaguzi.
- Kutoonyesha hasira na kuamua kutoka kwenye uongozi/chama.
- Kujifunza na kukubali tofauti miongoni mwa watu na pia kukubali kurekebishwa iwapo utaonekana umekosea.

- Kuchangia topics zinazotakiwa kuchangiwa kimawazo.
- Kutotawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na uongozi nnje ya uongozi.
- Kukubali kuacha uongozi pale itakapoonekana umeshindwa kutekeleza matakwa ya watu wote.

## 11.2 Muda wa Uongozi

- Kila kiongozi atachaguliwa wakati wa mkutano mkuu (March) na uongozi utadumu madarakani kwa muda wa miaka miwili (2) toka tarehe ya uchaguzi.
- Mkurugenzi Mtendaji ataendelea na uongozi bila kubadilishwa.
- Viongozi wapya watatakiwa kujitolea kwa muda wa mwaka mmoja bila Motisha iwapo hawajawahi kuwa viongozi.
  - Ikitokea kiongozi kutaka kujiudhuru kabla ya wakati, atatakiwa kutoa taarifa (kwa maandishi) wiki mbili kabla ya kujiudhuru.
    - Bodi ya wadhamini inaweza kuteua kiongozi wa muda kukaimu nafasi hiyo mpaka uchaguzi ujao.
- Kiongozi yeyote anaruhusiwa kuendelea madarakani iwapo hakutakuwa na kiongozi wa kujitolea katika sehemu husika.

## 11.3 Sababu za kusimamishwa Uongozi

### 11.3.1 Kiongozi atasimamishwa iwapo atafanya yafuatayo:

- Kutoheshimu uongozi/wanachama.
- Kutumia lugha isiyo sahihi.
- Kutokuwa na pesa kwenye akaunti ya chama kama akiba kwa muda wa siku zaidi ya 30.
- Kuleta mambo binafsi kwenye chama na kuanzisha malumbano yasiohusiana na uongozi.
- Kushabikia mambo binafsi na kuendeleza malumbano zaidi ya mara 3.
- Kutoonyesha mifano ya utendaji na kutawanya habari/sauti (siri) zinazohusiana na uongozi nnje ya uongozi.
- Kubadilisha mawazo tofauti na makubaliano ya viongozi (wengi wape).
- Kutochangia mada zinazotakiwa kuchangia zaidi ya mada 3.

### 11.3.2 Kiongozi atapewa warning zifuatazo:

- Kutaarifiwa kuwa amekosea na Mwenyekiti.
- Kuandikiwa barua na Mwenyekiti.
- Kukutana na wajumbe wote wa Bodi.
  - Atatolewa kwenye uongozi kwa muda wa siku 90 (miezi 3) na kurudishwa

- Atasimamishwa uongozi akirudia makosa na kutoruhusiwa kuwa kiongozi tena.

## IBARA YA KUMI NA MBILI

### 12. WAJIBU WA VIONGOZI WA KAMATI YA UTENDAJI

Viongozi wote watafanya kazi mara baada ya kuchaguliwa. Wote kwa pamoja watawajibika kama ifuatavyo:

12.1 **MKURUGENZI MTENDAJI -** (CEO)

- Kusimamia na kuangalia mwenendo wa chama na bodi.
- Kufanya kazi kwa karibu na Wenyeviti (Kamati & Bodi).
- Kutatua matatizo yatakayojitokeza kati ya Kamati na Bodi.
- Kusimamia ugawaji wa MOTISHA kwa viongozi wote kwa kuangalia mwenendo wa kazi wanazozifanya.

12.2 **MWENYEKITI** - (President)

- Kuongoza na kuangalia mwenendo wa chama.
- Kuongoza vikao vikuu vya chama na kutoa report ya vikao hivyo.
- Kuongoza vikao vya kamati ya utendaji na kutoa report za vikao hivyo.
- Kuweka kumbukumbu zote za vikao vya chama kwa usahihi.
- Kushughulikia masuala yote ya chama kama Mwenyekiti.
- Kufanya kazi kwa karibu na viongozi wote.
- Kuidhinisha badget ya chama kwa kushirikiana na Bodi ya Wadhamini.
- Kutoa idhini ya mwisho ya maamuzi ya chama.
- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti wa Bodi.
- Kutoa maamuzi wa mwisho iwapo kura zitagongana.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

12.3 **KATIBU/MHAKIKI** – (Secretary General/Reviewer)

- Kushughulikia na kuidhinisha shughuli yoyote inayohusu mwanachama.
- Kutoa taarifa zozote za mwanachama na matukio yote (shida/misiba).
- Kuwa na kumbukumbu za wanachama wote.
- Kufanya kazi kwa ukaribu na Mweka Hazina.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

12.4 **MWEKA HAZINA** – (Treasurer)

- Kukusanya michango ya chama kama itakavyokuwa imekubalika na kuhitajika.
- Kuandaa bajeti ya chama na kuidhinisha matumizi ya chama.
- Kukagua na kuidhinisha matumizi ya chama.
- Kutoa taarifa ya mapato kila mwezi na wakati wa kufunga shida/misiba.
- Kutoa pesa kwa wenye shida/misiba.
- Kutoa pesa kwa shughuli zinazohusu chama.
- Kutoa taarifa ya matumizi ya chama.
- Kuweka kumbukumbu sahihi za michango ya chama.
- Kuweka kumbukumbu na risiti za matumizi yanayohusu chama.
- Kuibua njia mpya za mapato ya chama.
- Kufanya kazi kwa karibu na Katibu/Muhakiki.
- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti na watia saini.
- Kuhakikisha nakala za upokeaji wa pesa zimejazwa kikamilifu na kuwa na sahihi zote.
- Kufile Income Tax IRS Form 990.
- Kuwa mwaminifu na kutotumia pesa za chama.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

12.5 **AFISA UHUSIANO – (**Public Relations Officer)

- Kukagua na kutangaza matangazo siku zisizokuwa za matangazo.
- Kutoa taarifa za chama kwenye mitandao ya kijamii.
- Kutangaza na kukaribisha wageni.
- Kutoa mafunzo kwa wageni.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

## IBARA YA KUMI NA TATU

### 13. WAJIBU WA VIONGOZI WA BODI YA WADHAMINI

Viongozi wote watafanya kazi mara baada ya kuchaguliwa. Wote kwa pamoja watawajibika kama ifuatavyo:

13.1 **MWENYEKIT**I (Chair of the Board)

- Kuongoza vikao vikuu vya Bodi.
- Kufanya kazi kwa karibu na Katibu na Wajumbe.

- Kushauriana na Katibu/Wajumbe na kutatua matatizo yatakayojitokeza kwenye chama.
- Kuandaa na kuhakikisha sheria zinapitishwa na wajumbe ili zitumike na chama.
- Kuangalia kwa umakini utendaji wa kazi kwa katibu na wajumbe wa Bodi.
- Kumsimamisha kiongozi wa Bodi, Kamati ya Utendaji/Mjumbe yeyote asiyefata sheria.
- Kushirikiana na Mwenyekiti Mkuu kwa kuhakikisha sheria na matatizo ya chama yanafanyiwa kazi.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

13.2 **KATIBU** (Secretary)

- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti.
- Kutoa taarifa za mikutano ya Bodi.
- Kuweka listi ya Wajumbe wa Bodi na kumbukumbu za vikao vyote vya Bodi.
- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti/Wajumbe
- Kuhakikisha nakala zote ziko sahihi/vizuri na tayari kwa kutumika pale zinapotakiwa.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

13.3 **WAJUMBE**

- Kufanya kazi kwa karibu na Mwenyekiti/Katibu.
- Kushiriki kikamilifu kwa kutoa michango na mawazo katika vikao na shughuli zote za chama.

## IBARA YA KUMI NA NNE

**14. WAJIBU WA VIONGOZI WA KLABU**

- Kuongoza na kuangalia mwenendo wa Klabu.
- Kuleta maoni ya nini kifanyike kwenye Klabu.
- Kushirikiana na Mwenyekiti Mkuu na kuamua kwa pamoja nini cha kufanya kwenye Klabu.

## IBARA YA KUMI NA TANO

**15. VYANZO VYA MAPATO YA CHAMA**

**15.1 Vyanzo vya mapato ya chama hiki vitakua kama ifuatavyo:**

- Ada ya uanachama ya kila mwanzo wa mwaka (April & Non refundable).
- Viingilio vya wanachama wapya kila mwezi (Non refundable).
- Harambee mbalimbali za kutunisha mfuko wa chama.
- Misaada kutoka kwa kampuni, watu binafsi, mashirika ya kitaifa na kimataifa yaliyo ndani na nje ya nchi.

15.2 Kwa kuzingatia ibara 15.1, wanachama wanauwezo wa kutoa njia mbadala ambazo zinaweza kutunisha mfuko wa chama, ila njia ziwe halali.

15.3 Pale itakapolazimu kufanyika ukaguzi wa mahesabu. Ukaguzi huu utafanywa na wakaguzi wenye sifa kulingana na sheria za Texas.

## IBARA YA KUMI NA SITA

**16. FEDHA NA UENDESHAJI WA AKAUNTI ZA BENKI.**

16.1 Kulingana na mwenendo wa chama, mapato yote yatakayopatikana katika chama yatahifadhiwa kwenye akaunti ya chama ambayo itakuwa chini ya Muweka Hazina, Mwenyekiti na Watia Saini wawili. Watia saini hao watakua na dhamana ya kutunza fedha hizo na kuhakikisha usalama wake.

16.2 Michango yote ya chama itawekwa kwenye akaunti ya chama na wanachama husika na kumkabidhi receipt/ujumbe Muweka Hazina. Mwanachama anatakiwa kutuma michango yote kupitia

Jina la Benki: Wells Fargo
Jina la Akaunt: Tanzania Sharing Association
Benki Akaunti Namba: 7975995742

**Zelle Information**
Jina: Tanzania Sharing or Tanzania Association
Telephine: (206) 602-0506
Benki Akaunti Namba: 7975995742

**Cashapp Information**
Cashapp: $TSA2025
Telephine: (206) 602-0506

16.3 Wanachama watapokea taarifa za mapato ya shida/msiba mara moja kwa mwezi (Kati ya tarehe 1-5) na wakati wa kufunga shida/misiba.

16.4 Mwanachama atapokea michango kwa kutumia njia tofauti tofauti zikiwemo Bank transfer/Checks/Cashier's Checks/Money Order/Paypal/CashApp/Western Union/Wave/World Remit.

16.5 Fedha zote zitatumika katika shughuli za kijamii zikiwemo shida/misiba itakayotangazwa na Muhakiki.

## IBARA YA KUMI NA SABA

**17. MICHANGO**

17.1 Ada ya uanachama $25 kila mwanzo wa mwaka (April & Non refundable).

17.2 Mwanachama atachangia shida/misiba pale taarifa ya mwanachama/ndugu itakayokubaliwa na Muhakiki na kutangazwa kwenye chama **(3,000/jumla ya wanachama hai)** ndani ya majuma mawili.

- Mwanachama atachangia misiba/shida 3 mpaka 5 ndani ya mwezi na sio zaidi ya $100.
    - Ikiwa zaidi ya misiba/shida 5 au $100, mwanachama atachangia misiba mingine mwezi unaofata.

17.3 Mwanachama atachangia pale taarifa ya kifo cha Mwanachama/Mtoto itakapotangazwa kwenye chama **(10,000/jumla ya Wanachama)** ndani ya majuma mawili.

- Mtoto wa chini ya miaka 21 aishio jimbo lolote ndani ya USA.
- Mwanachama atachangia misiba 2 mpaka 3 ndani ya mwezi na sio zaidi ya $200.
    - Ikiwa zaidi ya misiba 3 au $200, mwanachama atachangia misiba mingine mwezi unaofata.

17.4 Mwanachama asipochangia **shida/msiba 3** bila taarifa yeyote/isiojitosheleza, atakuwa amevunja sheria ya chama na hivyo atapelekwa kwa Bodi ya Wadhamini kwa maamuzi zaidi. Bodi ya wadhamini itamsikiliza na ikiamua kumtoa katika chama, basi hatorudishiwa pesa ya nyuma aliyokwisha changia.

- Shida/msiba wa kwanza na wapili atapewa **Ony**o na shida/msiba wa 3 atapelekwa kwemye Bodi ya Wadhamini kwa maamuzi zaidi.
    - Adhabu hizi zitaisha ndani ya mwezi na kuhesabika upya iwapo mwanachama atarudisha michango yote aliokosa kuchangia.
    - Mwanachama hataruhusiwa kurudi ndani ya mwaka mmoja na pindi atakapotaka kurudi atatakiwa kurudi kama mwanachama mpya.
- Mwanachama aliechangiwa, atatakiwa kurudisha pesa aliyochangiwa (Pesa aliochangiwa – Pesa aliochanga).

- Iwapo mwanachama atakataa kurudisha pesa au kugundulika ametoa habari za uongo
    - Mwanachama atachukuliwa hatua kisheria na kutangazwa kwenye vikundi vingine kama fundisho.
    - Mwanachama hataweza kusaidiwa tena katika shida/raha zake na TSA.

**Utangulizi:** Michango itabadilishwa iwapo kutahitajika na uongozi/wanachama.

## IBARA YA KUMI NA NANE

**18. MAFAO KWA MWANACHAMA**

18.1 Kufariki kwa mwanachama/mtoto wa umri chini ya 21 – **USD 10,000/$5,000/$2,000.**

- Viongozi watasaidiana na wasimamizi wa msiba katika shughuli nzima ya kumpumzisha mwanachama. Kiasi chochote kitakachobaki kitakabidhiwa kwa wahusika baada ya mwanachama kupumzishwa.

18.2 Kupata shida/msiba kwa ajili ya mwanachama na ndugu – **USD 3,000/$1,500/$500.**

18.3 Motisha kwa wanachama/viongozi watakaoleta misaada kutoka kwa kampuni, watu binafsi, mashirika ya kitaifa na kimataifa yaliyo ndani na nje ya nchi (10% ya kiasi watakacholeta).

18.4 Motisha kwa viongozi
$200 itatengwa kutoka kwenye kila tukio litakalolipwa na TSA kwa ajili ya uendeshaji na kusimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji.

18.5 Gharama za usafiri (mileage), chakula, malazi kwa viongozi wote iwapo watashughulikia kazi za chama.

18.6 Kutimiza miaka 50, 60, 70, 75, 80, 85, 90, 95, 100 kwa wanachama – $50 au $100 iwapo watakuwa na sherehe itakayoshirikisha wanachama.

18.7 Harusi za wanachama $100.

18.8 Kuhitimu shahada za juu kwa wanachama pamoja na watoto chini ya miaka 21.

- $25 kwa Sekondari (High School Diploma).
- $50 kwa Shahada ya kwanza (Associate & bachelor’s degree).
- $100 kwa Shahada ya juu/uzamili (Master’s & PHD).

18.9 Ukizingatia Ibara ya 18.1 & 18.2, mwanachama atapokea mafao yake

- Baada ya Muhasibu kuhakikisha kama mwanachama ana **$125** kwenye akaunti ya chama
    - Ikiwa chini ya $125 (Akiba tangulizi & ada ya uanachama), mwanachama atakabidhiwa **$1,500** na familia itasaidiwa **$5,000**.
    - Ikiwa ana **$0** kwenye akiba tangulizi (advance) ila ana **$25** ada ya uanachama, mwanacha atakabidhiwa **$500** na familia itasaidiwa **$2,000.**
    - Ikiwa hana pesa kwenye account, mwanachama/familia watachangiwa kihiari.

- Baada ya Muhakiki kuridhia na kutangaza shida/msiba.
- Baada ya kutoa taarifa za matumizi/upokeaji wa pesa, kutoa kitambulisho cha taifa na kutia saini mkataba wa kupokea pesa.

## IBARA YA KUMI NA TISA

**19. SHERIA NDOGONDOGO NA UREKEBISHAJI WA KATIBA**

19.1 Uongozi wa chama utatakiwa kutengeneza sheria ndogondogo za chama ili kuwezesha chama hiki kuendelea vizuri.

19.2 Sheria ndogondogo zote zitaanza kutumika mara baada ya kutungwa na kukubalika na wanachama kwa kuanza kutumika.

19.3 Ibara zinazounda katiba hii na sheria ndogondogo za chama zinaweza kufutwa na/au kurekebishwa baada ya nusu ya wajumbe wa chama kupitisha pendekezo hilo.

19.4 Sheria zozote zilizofutwa miaka ya nyuma, haziruhusiwi kurudishwa katika katiba.

19.5 Katiba hii inaweza kufanyiwa mabadiliko kila baada ya miaka 2 kwa kuongeza vifungu au kuboresha vilivyopo. Mabadiliko au marekebisho ya katiba yanaweza kufanywa kwa azimio la wanachama litakaloungwa mkono na 2/3 ya wanachama katika mkutano mkuu.

# IBARA YA ISHIRINI

**20. KUVUNJIKA KWA CHAMA**

Iwapo litajitokeza jambo lolote litakalopelekea chama hiki kuvunjika au kuvunjwa, azimio hilo la kuivunja chama lazima liwe limeungwa na 2/3 ya wanachama hai wa mkutano mkuu. Ili mkutano huo uweze kuwa halali, inabidi ¼ ya wanachama hai wa chama wahudhurie mkutano huo. Mara baada ya azimio hilo kupitishwa, utafanyika utaratibu wa kutathmini mali zilizopo. Iwapo kutakuwa na madeni, madeni hayo yatalipwa kwanza na mali zitakazobakia zitagawanywa kwa wanachama hai kwa usawa.

## MWISHO